# AFRI TWENDE

Kulitia moyo kanisa la Afrika katika kazi ya umisheni ulimwenguni

Jarida la 8, Toleo la 2

# MASUALA YA FAMILIA NA WITO WA UMISHENARI

## KUUTAWALA MVUTANO




AKINA MAMA WAZIBA PENGO

MAMBO YAWA MAZURI KWA REAGAN

WWW.AFRIGO.ORG/AFRITWENDE

# YALIYOMO








## 03 TAFUTA UWIANO

Wito wa umishenari unaweza kuleta mvutano kati ya kuwajibika kwa mtu kwa ajili ya familia yake na uaminifu wake kwa Kristo.

Dr. Chinedu Oranye wa Nigeria anashauri uwepo wa uwiano.

## 04 NIMEITWA: SIKO MPWEKE TENA

Ralambo Tiffanie alihisi kutelekezwa na watu wa familia yake. Baada ya kujifunza kuhusu umisheni na kuhudumu nchini Madagascar, sasa uhusiano wake na wao umekuwa bora kuliko hapo awali.

## 05 KUTUMIA FALSAFA YA 'UBUNTU'

Je, ni lazima wito wa umishenari uwatenge wamishenari na familia zao?

Falsafa ya Kiafrika ya Ubuntu inaweza kuwa jibu sahihi.

## 06 MAMBO YAWA MAZURI KWA REAGAN

Reagan Opoku Agyeman alijikuta yuko peke yake dhidi ya familia yake alipotangaza kutumwa kwake kwenda kuwa mmishenari. Ni nini kilibadilisha habari ya maisha yake?

## 08 WITO WA UMISHENARI NA WASIWASI WA FAMILIA

Kutimiza wito wa umishenari na kutimiza majukumu ya kifamilia linaweza kuwa jambo gumu kufanya.

Viongozi wa umishenari wanatoa majibu ya kina kwa maswali magumu.

## 11 AKINA MAMA WAZIBA PENGO

Akina Mama wa Msaada wa Nigeria wanasaidia watoto ambao wazazi wao wako mbali katika maeneo ya umisheni. Soma jinsi ilivyoanza katika tukio la maadhimisho na kile walichokifanya mpaka sasa.

© 2026 AFRITWENDE

AFRITWENDE ni chapisho lenye lengo la kuinua ufahamu, hamasa, mafunzo na kuamsha makanisa na watu binafsi katika kuelekea kwenye huduma ya umisheni ulimwenguni.

**Mhariri Mkuu:** Jesse Katabi Masolwa
**Masanifu:** Pilgrim Communications

**Picha kwenye jalada: Familia ya Mills, Ghana (Gheorge Oliver photography)**

Maoni yaliyoelezwa hapa katika makala mbalimbali katika Jarida hili si lazima yawe ya mchapishaji. Picha halisi hutumika mara chache. Majina ya bandia hutumika pale ambapo panahitajika kwa sababu za kiusalama.

www.afrigo.org/afritwende

# TAFUTA UWIANO

## NA CHINEDU ORANYE



Familia ni ya muhimu sana kwa Waafrika. Ukiondoa familia, sisi tunajiona sio watu. Familia zetu zenye wazazi na watoto na zile za wazazi, watoto na ndugu wengine zimeunganishwa, na hali hii mara nyingi huamua maamuzi mengi tunayofanya. Je, hili linaathiri vipi msimamo wetu katika umisheni na kama wamishenari?

Kwanza, Yesu anataka uaminifu wa dhati kutoka kwa wote ambao wanataka kumfuata, wakiwemo Waafrika. Katika Mathayo 10:37, anasema, "Yeye apendaye baba au mama kuliko mimi, hanistahili; wala apendaye mwana au binti kuliko mimi, hanistahili." Yesu alikuwa wazi kuhusu kipimo cha ufuasi, na wito wa kimishenari huanza na kumalizika kwa kumfuata Yesu. Kama Waafrika, lazima tukubaliane na ukweli huu. Hatuwezi kuruhusu wajibu wetu kwa familia utupokonye haki na fursa ya kumtumikia Yesu. Tumeshindwa wajibu wetu ikiwa tutaacha mapokeo ya familia zetu yabatilishe maagizo ya Yesu ya "kwenda kufanya wanafunzi."Kumfuata Yesu kutaathiri familia, na wakati mwingine, kunaweza kulazimu kufanya maamuzi magumu. Lakini, utii kwa Kristo ndio kipaumbele chetu cha kwanza.

**Ingawa uaminifu wetu kwa Yesu unapaswa kubaki bila mashaka, kuudhihirisha kwetu huo uaminifu hakupaswi kuchoma madaraja yanayotuunganisha na mitandao ya familia zetu**

Kwa upande mwingine, Yesu anawaambia Mafarisayo katika Mathayo 15:5-6, "...nyinyi mwasema, Mtu ye yote amwambiaye baba yake au mama yake, "Kicho chochote ambacho ungepata kutoka kwangu ni wakfu kwa Mungu; hana haja ya kumheshimu baba yake au mama yake.'... mmeibatilisha amri ya Mungu kwa mapokeo yenu." Yesu anathibitisha umuhimu wa kuheshimu familia. Hakukubaliana na ile dhana ya kwamba ukiroho unapingana na kujitoa kwa ajili ya familia. Yesu alibainisha wazi kwamba kutoheshimu familia ni kutotii amri ya Mungu. Umisheni wa kisasa, kwa bahati mbaya, umetufundisha kwamba kuacha familia ilikuwa ni kigezo cha kumtumikia Mungu; hivyo, vijana wengi wa Kiafrika kwa kizembe wametelekeza majukumu yao ya kifamilia katika harakati za kuokoa mataifa. Mwitikio huu wa kibinafsi na umimi umeziacha familia nyingi za kiafrka katika hali ya uadui dhidi ya Yesu na wito wake.

Tunapatanishaje misimamo hii miwili? Kama Waafrika, lazima tutafute uwiano kati ya kumfuata Yesu, kutumika kwenye umisheni, na kuheshimu familia. Ingawa tumeitwa kuyatoa maisha yetu ili kumfuata Yesu, tunapaswa kuendelea kujitoa kwa ajili ya familia zetu na kuzihudumia. Wakati uaminifu wetu kwa Yesu unapaswa kubaki bila mashaka, kuudhihirisha kwetu huo uaminifu hakupaswi kuchoma madaraja yanayotuunganisha na mitandao ya familia zetu.

Katika toleo hili la AfriTWENDE, fuatilia safari ya Reagan ya upinzani kutoka katika familia yake na hatimaye kukubalika kwake kwao na kuungwa mkono nao. Makala ya Mtazamo inatoa suluhu la Kiafrika juu ya njia panda ya familia ya mmishenari. Akina Mama wa Msaada huko Nigeria wanaonesha jinsi wale walio nyumbani wanavyoweza kusimama katika pengo la wamishenari wanaotumikia shambani. Toleo hili la AfriTWENDE na lisaidie wamishenari na familia zao kuelewana na kusaidiana, na kuutia moyo Mwili wa Kristo kusimama pamoja na wamishenari na familia zao.

*Dr. Chinedu Oranye ni Mwalimu wa Biblia kutoka Nigeria, mwandishi, mshauri wa mambo ya uongozi, na mchungaji. Huduma yake imempeleka katika nchi zaidi ya 30, akishirikisha Injili ya Kristo ya upendo na imani kwa waliopotea na kwa Kanisa. Anafanya kazi na shirika la Calvary Ministries (CAPRO) na Haggai International. Ni mme wa Taiwo na wana watoto watatu. chinedu.oranye@gmail.com.*

# NIMEITWA: RALAMBO TIFFANIE

# SIKO MPWEKE TENA

## KAMA ILIVYOSIMULIWA KWA MERCY KAMBURA


Tiffanie Ralambo

Nilitiliwa shaka nilipowasili kwa mara ya kwanza kama mmishenari hapo Kisiwani. Sikujua kwamba baadhi ya wanawake wa Kimalagasi ambao waliofika kabla yangu. Ilikuwa vigumu kuishi nikiwa msichana mmishenari wa Kimalagasi ambaye hajaolewa. Nilipata shida sanakupata marafiki, lakini ilinibdi nikae tu kwa ajili ya Injili.

Kama mzaliwa wa katikati katika familia ya watoto saba, nilikuwa mtoto wa bango la kujihurumia. Kuambiwa maneno mazuri (ya uthibitisho) na kuwa na wakati mzuri ni jinsi ya kuonyesha upendo, na nilikuwa sipati dozi zake. Familia yangu ilikuwa na uhusiano wa karibu nami, lakini akili yangu changa ilihisi kwamba nilikuwa miongoni mwa walio wadogo zaidi katika familia yangu. Licha ya jitihada zao za kunipa upendo, bado nilihisi hautoshi. Hata hivyo, kunijali kwao kulinifanya niendelee nilipojitolea kuwa mmishenari. Licha ya kuwa msichana ambaye sijaolewa, familia yangu ilikuwa na uhakika kwamba Bwana alikuwa amenituma.

Nilimwamini Bwana wakati nikiwa chuo kikuu. Nilihudhuria ushirika wa ushirika wa Biblia wa Chuo Kikuu (yaani University Bible Group kwa kifupi UBG), na mafunzo ya Biblia yalinivutia. Sikuwa nimewahi kusikia Neno la Mungu kwa uwazi namna hiyo. Licha ya kukulia katika nyumba ya Kikristo, sikuwa bado mtoto wa Mungu, kwa hiyo nilitoa maisha yangu kwa Yesu.

Bwana alinifanya upya na kunipa furaha; sikuwa na hasira tena na familia yangu. Nilipoanza kuzaa matunda, walishangaa kwamba nilikuwa nikipendezwa na mambo ya Kristo. Nilisikia kuhusu umisheni kupitia Usharika wla Biblia wa Chuo Kikuu (UBG). Nilishuhudia jinsi vijana walivyokuwa wanawaka moto kwa ajili ya Mungu. Nikasema, "Yesu, nitakapokua katika imani yangu, nitaenda pia mahali fulani Madagascar kuhubiri Habari zako Njema."

> Familia yangu inaniunga mkono na haijawahi kupinga umisheni ambao ninaufanya.

Nilianza kushiriki katika umisheni na kujifunza kuhusu maisha ya umishenari. Baadaye nilienda kama mmishenari chini ya shirika la kimishenari la AIM hadi visiwa vya Madagascar ili kutumika miongoni mwa watu ambao hawajafikiwa.

Eneo la umisheni lilikuwa na mambo mengi ya kushtua yaliyokuwa yakiningoja. Sikuwa na muda wa kujiandaa. Nilijifunza kila kitu nikiwa tayari shambani, hata vitu ambavyo ningepaswa kujua kwa nadharia. Nilikuwa Mmalagasi pekee kwenye timu yangu, na upweke ulianza kutanda. Wakati fulani, nilitaka kukimbilia nyumbani na kulia. Nilipakumbuka nyumbani, na pia sikuwa na ufadhili wa kutosha wa kifedha. Baada ya mwaka mmoja, nilirudi nyumbani kwenye sherehe kama ya mwana mpotevu kutoka kwa familia yangu.

Kurudi nyumbani, nilianza kufanya kazi na shirika lisilo la kiserikali linalosaidia wanawake. Tuna mradi unaolenga kuhubiri Injili kwa Wahindi hapa Madagascar. Nimekuwa nikimfundisha mwanamke wa Kihindi mwenye asili ya Kiislamu ambaye ndiye mwamini peke yake katika familia yao. Nimeuelewa moyo wa Mungu kwa ajili ya mataifa na sasa ninaona zaidi ya upendeleo wa kitamaduni.

Maisha yangu ni kwa ajili ya Bwana, na ninachagua kuyatumia kwa kitu ambacho kitadumu milele.

Bwana akikuita, nenda. Usisubiri. Sijisikii mpweke tena. Bwana aliniweka katika familia yake ya mbinguni, na uhusiano wangu na familia yangu ya hapa duniani umekuwa bora kuliko ulivokuwa hapo awali. Dada zangu wanatamani zaidi kuwa na uhusiano na Yesu. Familia yangu inaniunga mkono na haijawahi kupinga umisheni ambao nimeufanya.

**OMBA KWA AJILI YA:**

- Hatua zangu zinazofuata; moyo wangu unatamani kurudi kwenye huduma ya umisheni. Omba kwamba Bwana aniongoze katika kila nilifanyalo.
- Familia yangu na mimi tukue katika upendo wetu kwa Yesu Kristo.
- Jamaa zangu ili wamjue Bwana.

www.afrigo.org/afritwende

# WITO WA KIMISHENARI NA FAMILIA
# KUTUMIA FALSAFA YA 'UBUNTU'

NA TIMU AFRITWENDE

Je, ni lazima mmishenari aitelekeze familia yake ili aitikie kiukweli wito wa Mungu wa kuwafikia waliopotea? Katika Bara lote la Afrika, kizazi kipya cha wamishenari wa Kiafrika kinaenda kwenye maeneo ya umisheni, na familia zao hazielewi kabisa sababu zinatolewa kila wakati. Inaweza kuonekana kuwa ni ubinafsi, hasa ikiwa familia ilijitoa muhanga katika kusomesha na kulea huku ikitarajia thawabu baadaye.

## Wito wa umishenari

Wengine wameitwa katika umisheni kwa njia ya ajabu kama vile ilivyomtokea Paulo huko Dameski. Kwa wengine, ni msukumo unaoongezeka tu unaoonesha kwamba Mungu anataka mwelekeo tofauti kwa ajili yao. Bila kujali njia ambayo mtu au wanandoa hatimaye wanatambua kwamba Mungu anataka waende mahali na kutumika kama wamishenari. Hili linapaswa kuthibitishwa na washauri wa kiroho wanaoaminika na waliokomaa.

Kwa wakati huu, familia inaarifiwa kuhusu uamuzi huo, ambao unaweza kusababisha uthibitisho wa hofu mbaya zaidi walizonazo: mtoto wao atakuwa ombaomba, anaweza kuuawa katika nchi ya kigeni, au kupata watoto ambao hawatajua kamwe babu na bibi zao. Uwekezaji wao huo wa awali kwenye elimu sasa unaonekana kuwa si kitu. Kwa bahati mbaya, mchungaji wa kanisa la mahali wakati mwingine anaweza kuwa mojawapo ya vikwazo vikubwa kwa mmishenari, kwa madai kuhusu mahitaji ya huduma mahali walipo, kutilia shaka wito, au hofu yake mwenyewe kuhusu pesa kuondoka kanisani kwenda nchi ya kigeni. Majibu haya yanahuzunisha kwa mtu ambaye tayari anahangaika, labda kwa miaka mingi, kuhusu mipango ya Mungu ya umisheni kwa ajili yake.

## Ubuntu na umisheni

Hebu tuangalie njia mbadala kwa kutumia falsafa ya Kiafrika ya Ubuntu. Inahusiana na msemo wa Kizulu "Umuntu ngumuntu ngabantu," ambayo ina maana kwamba mtu ni mtu kupitia watu wengine. Je, hatuwezi kutumia hili kwa wito wa umishenari? Je, inawezekana kwamba Mungu ameelekeza wito huo kwa mtu binafsi na jamii inayomzunguka?

Vipi ikiwa mafanikio ya umishenari yatachukuliwa kuwa ni mafanikio ya jamii nzima badala ya mafanikio ya mtu mmoja ambaye anafanya kazi katika shamba la mavuno (eneo la umisheni)? Hebu tupige picha ya jamii inayosikia wito wa Mungu wa wapendwa wao. Wanaomba kwa ajili ya uthibitisho wa wito wao, wanahakikisha kwamba wameandaliwa kwa mafunzo ipasavyo, na wanasaidiwa kiuchumi vyema wanapokuwa wakihudumu katika eneo la umisheni. Wanamkaribisha mpendwa wao anaporudi nyumbani na kumtia moyo anapojitayarisha kurudi shamabani. Ndugu wanakusanyika karibu na wanafamilia ambao, wakati mmishenari hayupo, wanahitaji msaada. Hii haingekuwa udhihirisho halisi wa Ubuntu? Soma jinsi ambavyo familia na jamii ya Grace* walivyoweza kufanya vilevile.

## Simulizi ya Grace

Nilipowajulisha wazazi wangu kwa mara ya kwanza kuhusu wito wangu wa umishenari, baba yangu alitabasamu. Mama yangu alisema, "Ni pendeleo kumtumikia Bwana." Hawakuwahi kuhoji nia yangu wala kunivunja moyo. Kulikuwa na nyakati ambazo sikuwa na uhakika kuhusu mapenzi ya Mungu, lakini sikuzote walikuwa tayari kuzungumza na mimi na kuomba pamoja nami nilipohitaji.

Kabla sijaja kwenye eneo la umisheni niliunda kikundi cha maombi ili kuniombea kila wiki. Wazazi wangu walishiriki mfululizo. Kaka yangu aliliratibu kundi hili baada ya mimi kwenda shambani. Niliacha kazi yangu ili kujitayarisha kwa ajili ya kazi ya umishenari, na wazazi wangu katika uzee wao walinihifadhi kwa mwaka mzima. Hawakuwahi kulalamika juu ya hali yangu ya kutokuwa na uwezo wa kusaidia katika kukidhi mahitaji ya familia. Badala yake walinipa kiasi kikubwa cha pesa kwa ajili ya eneo la umisheni.

Niliacha kazi yangu ili kujiandaa kwenda katika maeneo ya umisheni, na wazazi wangu wa wazee tulienda pamoja nao kwa muda wa mwaka mmoja. Walinihudumia vizuri kwa mahitaji yangu na hawakuwahi kulalamikia hali ya kutokuwa na uwezo wa kukidhi mahitaji ya nyumba. Bali walinipa kiwango fulani cha fedha kwa ajili ya kujikimu nikiwa katika huduma.

Takriban watu 80 walihudhuria katika siku ya ibada yangu ya kutumwa shambani. Familia yangu yote ilikuwepo—wazazi wangu, kaka yangu, dada yangu, mume wake na watoto wao watatu. Marafiki zangu, wanafunzi wenzangu wa zamani, washirika wa kanisa, wafanyakazi wenzangu wa zamani, na viongozi wa umisheni pia walikuwepo. Walizungumza maneno ya uthibitisho juu yangu na kunibariki. Wanandoa fulani ambao ni wamishenari walinipa begi. Rafiki mmoja alikuja nyumbani kunisaidia kupanga mizigo yangu. Mmiliki wa biashara mmoja aliniongeza kwenye orodha yake ya malipo ili kunitumia pesa kila mwezi kama mmoja wa wafanyikazi wake.

Msaada wa kifedha niliopokea ulinitia nguvu kutimiza wito wangu wa kimishenari. Maneno ya baba yangu katika siku ya ibada ya kutumwa shambani yanaelezea moyo ulioko nyuma ya kila msaada nilioupokea kutoka kwa kila mtu—"Kama vile Mariam, mama yake Yesu, tunahisi kuheshimiwa sana kwamba Bwana alichagua familia yetu kwa kazi hii kubwa." *https://bit.ly/3NAioi9

# MAMBO YAWA MAZURI KWA REAGAN

NA KATE AZUMAH



**Reagan na wanafunzi wake wa huduma ya michezo**

Regani alikuwa hajawahi kutoka nje ya mji wa Kumasi. Siku ambayo Reagan alipanda basi kutoka Kumasi kuelekea eneo la umisheni mbali na nyumbani kwao ilikuwa siku ya kipekee. Alipofika Tamale, aligundua kwamba basi la kwenda Gbintre lilisafiri mara moja tu kwa siku. Hakulikosa, lakini alitamani angalau angekuwa amelikosa. Kwanza, basi lilitikisika vibaya sana! Kisha mvua ikanyesha, na licha ya kuwa ndani ya basi, lakini alilowana mwili mzima.

Muda uliokuwa umepangwa kufika ilikuwa ni saa 3 usku badala yake wakafika saa 6 za usiku wa manane. Alilala huko Gbintre na kuendelea na safari siku iliyofuata. Alikuwa akitarajia gari zuri ambalo lingemsafirisha yeye na mwenzake, Joseph, hadi kule wanakokwenda. Badala yake, walipanda kwenye baiskeli ya miguu mitatu isiyo na paa pamoja na wanawake wa sokoni ambao walizungumza lugha ngeni. Reagan anasimulia, "Hatimaye tulipofika Tuna, kijiji hicho hakikuwa na umeme. Usiku, giza lilikuwa nene sana sikuweza kuona nyuso za watu. Mama yangu alikuwa sahihi. Hapa ni mahali pa mateso, na sikupaswa kuja kamwe."

## Wito wa Reagan

Reagan Opoku Agyeman alihitimu shahada ya Usimamizi wa Biashara kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Kwame Nkrumah huko Kumasi, Ghana. Uamuzi wake wa kujisajiri kuwa mmishenari wa shirika la Operation Serve ulitokana na ushawishi wa rafiki yake, Razak. "Nilipokuwa nikimaliza shule, Razak aliniambia kuhusu fursa ya kufanya kazi ya umisheni wakati nikiwa Kwenye Mpango wa Huduma ya Kitaifa. Niliamua kuliombea jambo hilo. Sikuona maono yoyote au kusikia Bwana akizungumza, lakini niliamua kwenda kwa utii rahisi."

> Mama alikasirika; Baba, binamu, shangazi, na bibi walipinga.

## Wasiwasi wa familia

"Nilijua ningewaambia wazazi wangu naenda kufanya umisheni, jibu lao lingekuwa 'hapana' moja kwa moja. Kwa hiyo, nilipanda wazo akilini mwao kwamba kwa kuwa nilikuwa nimebobea katika Usimamizi wa Kilimo Biashara, kutumika Kaskazini kungekuwa faida ya kitaaluma. Mama yangu alisema atakuwa radhi na hilo."

Utumaji ukafika na Reagan alitumwa katika kijiji cha mbali cha Tuna katika wilaya ya Bunkpurugu katika mkoa wa kaskazini Mashariki. "Mama alikasirika; Baba, binamu, shangazi, na bibi walipinga. Dada mdogo wa Mama yangu aligombana na mimi na kusema hataniruhusu niende. Rafiki mmoja aliniuliza kwa nini nilikuwa mpumbavu hivyo. Uhasama ulikuwa dhahiri. Niliwaambia ni kwa mwaka mmoja tu, lakini hawakuridhika."

"Kwa mara ya kwanza maishani mwangu, niliamua kusimama mwenyewe. Niliwaambia nina umri wa kutosha kufanya maamuzi yangu mwenyewe." Reagan aliondoka nyumbani kwa muda wa wiki sita za mafunzo ya umisheni. Familia yake haikumzuia, lakini shida zake hazikuisha. "Nilipokuwa shule ya umisheni, Baba alinipigia simu alfajiri moja, na kuniomba nirudi nyumbani. Alikuwa akiongea kwa hisia sana."

Mama wa Reagan, Mama Anna, anaeleza, "Hakuna hata mmoja wetu aliyefurahishwa na habari hizo.

Kaskazini kulikuwa na hali tete, na tulihofia usalama wake." Baba yake Reagan pia alitarajia mzaliwa wake wa kwanza angepata kazi nzuri na ili kuisaidia familia kifedha.

## Maisha ya umishenari

Reagan alifundisha katika shule ya msingi ya Tuna, aliendesha huduma kwa watoto, aliratibu ibada za kanisa katika jamii nyingine, na kupitia huduma ya michezo, aliwafuasa wavulana wengi ambao mwanzoni ilikuwa vigumu kuwafikia.

Siku moja, Reagan na Joseph walikuwa wakivumilia joto kali nyumbani wakati Eliya alipoingia ndani kwa ghafla. Mkewe alikuwa akisumbuliwa na homa kali. Walienda pamoja naye na kumwombea. Walipokuwa wakiomba, nguvu za Mungu zilimshika na akaanza kutokwa na jasho. "Mbele ya macho yetu, aliponywa papo hapo! Sikuwa mtu wa kiroho sana, kwa hiyo nilishtuka. Iliniingia moyoni kwamba Mungu hakunileta hapa kwa ajili ya kujifurahisha, bali kwa ajili ya umisheni wa kweli." Huu ulikuwa mwanzo wa shuhuda nyingi huku watu wengi wakimiminika kuja kwa ajili ya maombezi.

Walimuombea Sala ambaye alitaka kupata mtoto. Alipojifungua, aliwaomba wampatie jina. "Tulimwita Muujiza," Reagan anasema. "Mwanamke mwingine aliye na kifafa alikuja kutoka Kusini kutafuta matibabu kwa mganga wa kienyeji huku Kaskazini. Tulimwomba aje kijijini kwetu kwa ajili ya maombezi. Siku iliyopangwa, kijiji chake chote kilikuja pamoja naye. Walitaka tuwaombee pia. Yule Mwanamke sasa ni mzima kabisa."

Wanaona kwamba kitu kizuri kimetokea ndani yake.



**OMBA KWA AJILI YA**

- Jamii za Wagonja zilizofikiwa kwa uchacheilli wamjue Kristo.
- Reagan na wamishenari wote wanaowafikia Wagonja ili Mungu awalinde.
- Neema ya pekee ya Mungu na amani kwa wazazi wa wamishenari wanaohudumu katika maeneo ya mbali.

Wakati alipokuwa nyumbani kutoka eneo la umisheni, Reagan alishirikisha shuhuda hizi kwa familia yake. Walianza kuacha kumsumbua, lakini walimkumbusha ahadi yake kwamba ilikuwa ya mwaka mmoja tu.

Reagan alipitia nyakati ngumu pia. Katika siku yake ya kwanza akiwa kwenye eneo la umisheni, alikuwa mgonjwa sana. Alipompigia simu mama yake akasema, "Njoo nyumbani. Tutakuhudumia." Reagan alibaki hakuenda. Kuwasiliana kwa simu kulikuwa kunakatisha tamaa. "Mahali pekee ningeweza kupata mtandao ilikuwa karibu na mti fulani. Ukitembea kidogo tu na mtandao unapotea." Mama Anna analalamikia hili kuwa ni wasiwasi mwingine kwa familia. "Hatukuweza kumpigia simu kwa wakati wowote tulipotaka. Ilibidi tumsubiri yeye ndo atupigie."

## Msaada kwa familia

Ingawa alipata kipato kidogo, Reagan alituma pesa kwa wazazi wake na ndugu zake mara kwa mara. Walifurahishwa na jitihada zake. Baada ya kutumika mwaka mmoja na shirika la Operation Serve, alijiunga na shirika la OneWay Africa kama mmishenari wa wakati wote. Kwa sasa yuko katika mwaka wake wa nne, na anasafiri kwa pikipiki yake akionyesha Filamu ya Yesu miongoni mwa jamii za Wagonja zilizofikiwa kwa uchache kaskazini mwa Ghana.

Familia ya Reagan sasa inaomba kwa ajili yake na kusaidia huduma yake kifedha. Wanaona kwamba kitu kizuri kimetokea ndani yake.

## Mawazo ya mama

Wasiwasi wa usalama wa Reagan haukumpa Mama Anna utulivu. Siku hizi, anasema, "Baadaye, nilitafakari na kuomba. Niligundua Mungu ndiye anayemlinda na sio sisi. "Tunafurahi kwamba anapata kipato cha kutosha kujikimu. Kuna wahitimu wengi wasio na kazi ambao bado wanategemea wazazi wao. Umisheni ni kazi nzuri, kwa hiyo tunamuunga mkono."

Mama Anna aliharibikiwa mimba nane kabla ya Reagan. Anatambua mkono wa Mungu juu yake, na hapingi. Huwashauri wazazi akisema: "Kumwachilia mtoto ayaendee yasiyojulikana si rahisi, lakini huna uwezo wa kumlinda. Wangeweza kuchagua njia ambayo ingekuletea matatizo na maumivu ya moyo. Wakichagua umisheni, waombee na uwaunge mkono."



Wazazi wa Reagan

www.afrigo.org/afritwende



PICHA: PEACE ALBERTO ITERITEKA

# WITO WA UMISHENARI NA WASIWASI WA FAMILIA

## MASWALI MAGUMU NA MAJIBU YENYE KINA

Umeitwa kutumika kama mmishenari, lakini wasiwasi wa kifamilia unatishia kukuvuta kwenda njia nyingine. Je, unatokaje kwenye hiyo njiapanda? Tumekusanya ushauri kutoka kwa viongozi wa umisheni ili kushughulikia baadhi ya masuala ya kawaida ya familia ambayo hujitokeza unapoamua kutumika kama mmishenari.

**Swali: Nimeitwa kuwa mmishenari katika nchi ya mbali, lakini wazazi wangu ambao kwa sasa ni wazee wanahofia maisha na usalama wangu. Pia wanahitaji uwepo wangu na msaada wa kifedha kutoka kwangu. Wanapendelea nisiende. Je, ninashughulikiaje wasiwasi wao na kupata baraka zao?**

Hili ni swali la kumtii Mungu na kuwatii wazazi. Huwezi kuliasi Neno la Mungu linalosema, "Yeye aipendaye nafsi yake ataiangamiza, lakini yeye anayeitoa kwa ajili ya Bwana ataipata" (Yn. 12:25). Wakati huo huo, huwezi kuwapuuza wazazi wako na kuondoka kwenda kwenye eneo la umisheni. Kuwatii na kuwaheshimu wazazi ni sehemu ya injili, na pia ni tendo la ibada.

Wasiwasi walio nao wazazi wako wazee ni wa kweli, lakini unamtumikia Muumba wa ulimwengu mzima, naye anaweza kukulinda wewe na familia yako. Wasaidie waelewe kwamba Mungu ndiye anayetuangalia na kutuweka salama. Watie moyo wakusaidie kwa kuombea usalama wako. Hata kama mabaya yatatokea na ukafa kwenye eneo la umisheni, ni bora kufa ukiwa unamtii Bwana kuliko kufa ukiwa haumtii. Ipe familia yako ushahidi wa kivitendo unaoonesha kwamba hutaacha kuwa mwana galifu na maisha yako. Waambie kuhusu ujuzi na mafunzo ambayo umepata ili kujilinda ikiwa uko hatarini. Wahakikishie kuwa teknolojia itakufanya uendelee kushikamana nao. Wasiliana nao kwa bidii, hata ikimaanisha kusafiri hadi mahali unapoweza kupata mtandao mzuri.

Biblia inasema tusipowatunza wa nyumbani mwetu, sisi ni wabaya kuliko wasioamini. Hata tukiwa katika eneo la umisheni au la, ni wajibu wetu kuwatunza; kutumikia kama mmishenari haimaanishi kukataa wajibu huu. Tafuta mwongozo wa Mungu na uweke pamoja mipango halisi ya kushughulikia mahitaji yao. Unaweza kupanga na viongozi wako wa umisheni kuhusu kupata usaidizi kwa ajili ya kuwatunza, au kupata mtu wa kuwatunza ukiwa mbali. Ikiwa wazazi wako bado wana msimamo mkali, tafuta viongozi wa Kikristo wanaoheshimika ili kuzungumza nao. Omba katika hatua hizi zote, na uwe na subira. Hakikisha kwamba wazazi wako wana amani ipasavyo kabla ya kuondoka kwenda katika eneo la umisheni.

**Swali: Ndugu zangu walioko kijijini walichangia kufadhili elimu yangu hadi ngazi ya chuo kikuu kwa sababu nilikuwa mwanafunzi niliyeonesha matumaini. Walitarajia nipate kazi nzuri baadaye na niweze kuwatunza ndugu walio wadogo zaidi wa familia yetu. Sasa ninahisi kuitwa kuwa mmishenari na sina budi kuomba msaada wa kifedha mimi mwenyewe ili niweze kufanya kazi ya umisheni. Je, nisaidie familia yangu au niitikie wito?**

Itikia wito wa Mungu (Mt. 6:33). Biblia inatuamuru tuwatunze ndugu zetu, lakini tarajio hilo la familia halina uhalisia. Je! kuna uhakika gani kwamba baada ya shule, utapata kazi ambayo inalipa vya kutosha kumtunza kila mtu? Unaweza pia kuanzisha familia yako mwenyewe.

Hii haimaanishi kwamba usiizingatie familia yako. Bado unaweza kuwatunza kwa kuwaombea, kuwapa ushauri mzuri (sio mara zote kuhusu pesa pekee), na kuwapa mahitaji ya kimwili na ya kifedha. Kwa maombi fanyia kazi mchakato huo, na wafahamishe kile unachoweza kufanya. Labda unaweza kumtunza ndugu mmoja amabye ni mhitaji au tegemezi kwa takriban miaka mitano, au wawezeshe baadhi yao kuanza biashara au kupata kazi au kujifunza ufundi. Kwa heshima, wape uhakika kwamba utafanya kile ambacho Biblia inakuagiza kufanya, lakini pia wajulishe kuwa huwezi kumtunza kila mtu.


Ishaka Ali

Waonyeshe kwamba umisheni ni wito unaostahili. Wakati mwingine mtazamo wetu wenyewe wa kizembe katika kuwasilisha kazi ya umishenari hutoa mvuto usiofaa na kuwafanya wawe na wasiwasi. Bwana anasema mtenda kazi anastahili ujira wake. Waeleze kwamba utalipwa; unaweza usijue jinsi gani, lakini utapata thawabu yako. Tembea kwa unyenyekevu ukipitia ngazi zote za mamlaka katika familia yako, na ombea mchakato mzima.

**Swali: Watoto wetu walizaliwa na kukulia katika eneo la umisheni la ugenini ambako walijifunza lugha na desturi za kundi (kabila) la watu tofauti. Mwingiliano wao pekee na wanafamilia wengine umekuwa ni kupitia mikutano michache ya mtandaoni. Tunajiandaa kuwapeleka nyumbani kwa mara ya kwanza baada ya miaka 15. Tunawezaje kufanya uwe wakati wa faraja na wa kuridhisha kwao na kwa familia nzima?**

Tafuta kujua kama kuna wanandoa wengine wako katika hali kama hiyo na jadili ni nini ambacho wamegundua kinachoweza kuwa cha msaada. Wakati huohuo, watayarishe watoto mapema kuhusu mambo ya kutarajia mnapoenda kuwatembelea ndugu huko nyumbani. Jambo moja ambalo linaweza kusababisha maumivu kwa familia huko nyumbani ni pale watoto wa wamishenari wanapokuwa hawawezi kuzungumza lugha ya nyumbani. Huenda familia ikahisi kwamba utamaduni wao unasahauliwa au unawekwa kando kwa ajili ya wengine. Ili kusaidia katika hali hiyo, wafundishe watoto wako salamu, ishara, na maneno yanayofaa kuongea na babu na bibi na ndugu wengine wa familia. Zungumza nao kuhusu utamaduni wako—chakula, lugha, mazingira ya familia, shughuli za kiuchumi—mambo mazuri na mabaya ili kuepuka mshtuko wa kitamaduni.

Isaidie familia yako kule nyumbani kuelewa kwamba watoto wako ni watoto wa wamishenari, kwa hivyo huenda mwingiliano wao nao usiwe rahisi. Unaweza pia kuelekeza familia yako kuhusu mazingira ambayo watoto wako wamekulia, ili waweze kuwachukulia na kuwasaidia.

---

*Mvutano kati ya wito wa kimishenari na masuala ya familia ni jambo la kawaida kwa wamishenari wa Kiafrika. Ukijikuta uko katika hali hii, hauko peke yako. Peleka haja zako mbele za Bwana kwa maombi na utafute ushauri wa kimungu na kutiwa moyo kutoka kwa wale wanaoelewa eneo hilo. Usisite kuomba msaada kutoka kwa ndugu wa kiume na wa kike katika Kristo wanaoweza kukusaidia. Mungu alijua utakabiliana na nini akikuita. Mwamini yeye akusaidie kulitii Neno lake kuhusu wito wako na wajibu wako kwa familia yako. Inaweza isiwe rahisi, lakini Mungu ni mwaminifu.*



# MATAMANIO YA DHATI KWA MAMA

## NA BISHOP MUSSA M. MAGWESELA

Miaka mingi iliyopita, Elkana Chubugu kutoka Ntaza, alimkiri Bwana kupitia Wamisheni na akakua katika Imani. Aliendelea kukua katika safari yake ya kutembea na Bwana Yesu Kristo akiwa Mwinjilisti na kiongozi wa Kanisa mlei katika Kijiji chake na vijiji jirani. Bwana aliiheshimu huduma yake. Miongoni mwa watu aliowaleta kwa Yesu Kristo kupitia ushuhuda wake ni Ganagana Mboje ambaye alimwamini Bwana Yesu akiwa na umri wa miaka 14. Kisa hiki ni kumhusu mtumishi huyu wa Mungu ambaye baadaye alikuwa mchungaji wa Africa Inland Mission.

Ganagana Mboje alikuwa mtu wa kwanza nyumbani kwao kumfahamu Bwana Yesu Kristo. Baba yake mzazi alifariki wakati akiwa kijana mdogo. Hali hii iliongeza majukumu mabegani mwake kwa ajili ya mama yake na wadogo zake akiwa ni mzaliwa wa kwanza. Ingawa hakufanikiwa kusoma katika mfumo rasmi wa elimu nchini Tanzania, aliuelewa ujumbe wa injili aliousikia kupita kwa Elkana Chubugu. Watu wa Ntuzu si rahisi sana kuyapokea mambo ya Kristo kama ilivyo kwa mtu wa tabia ya asili, kwa maana kwao ni upuzi. Ganagana alikuja kuwa mfuasi na mwanafunzi mwaminifu wa Kristo kupitia mikono ya Elkana Chubugu.



Doto Masunga

Sakwe, kijiji cha Elkana na Ganagana, ni jirani na mji wa Bariadi. Ganagana aliondoka nyumbani kwenda Bariadi kutafuta kazi. Kazi pekee ambayo angeweza kuipata ilikuwa ni kusaga unga. Ganagana, kupitia kazi hiyo alitegemewa kuwahudumia mama yake, wadogo zake na familia yake yote mahitaji muhimu. Bwana alikuwa akifanya kazi ndani ya Ganagana kwa njia ambayo hapana mtu aliyeweza kufahamu. Moyo ulikuwa ukimwaka ndani yake. Alikuwa akiomba awe mhubiri wa Injili. Shauku yake ilikuwa ni kufahamu kuhubiri. Ni neno la kumshukuru Mungu kwa vile Roho alimwezesha, yeye mwenyewe alijifunza kusoma na kuandika.

Aliamua kuacha kazi yake mwaka 1983 akajiunga na Chuo cha Biblia, Majahida. "Doto, mtoto wako amefanya uamuzi mbaya." Kama kawaida, ndugu na majirani walimcheka mama yake na Ganagana. "Uamuzi huu wa mwanao utaifanya familia yako yote iendelee kuwa maskini maisha yote."



Andrew na mzee wa Masaai

Walimdhihaki mama mzazi. Ganagana alibeba wajibu mkubwa sana wa familia. Aliwajali na kuwahudumia mahitaji yao ya kila siku. Kwa sababu hiyo kuacha kazi kulikuwa na maana ya kukata vyanzo vyote vya uchumi kwake mwenyewe, kwa mama yake, na kwa ndugu zake. "Lazima nijifunze kuhubiri." Ganagana alijitia moyo.

Muhula wake wa kwanza Majahida haukuwa rahisi. "Irudie kazi yako, mwanangu. Unayafanya maisha yangu yakose tumaini." Doto, mama yake alisisitiza. Mama alijitahidi kumzuia Ganagana asisome masomo ya Biblia. Mwinjilisti Elkana Chubugu pamoja na baadhi ya waalimu walijaribu kadri ya uwezo wao kumtuliza mama yake. Haikuwa rahisi. Mama aliendelea kulia akiamini kwamba mtoto wake amefanya uamuzi mbaya. Ganagana hakurudi nyuma. Alipohitimu alibaki chuoni kutumika akiwa mwinjilisti, kusimamia mashine ya kusaga unga pamoja na kuwa dereva. Mungu alimheshimu. Mboje, kama alivyokuja kufahamika, alimwoa Ephron kwa njia ya pekee sana. Mama yake na ndugu zake walifurahia sana vile mambo yalikuja kubadilika. "Bwana asifiwe sana kuwongoza mwanangu kufanya uamuzi sahihi." Mama yake alisema. "Ndugu pamoja na jirani zangu hawakunishauri vizuri." Mama alifariki akiendelea kumsifu Mungu.

Mboje alijaliwa kuwa mhubiri mzuri. Roho aliibariki huduma yake ya Injili hata miongoni mwa Wamasai ambako alitumika kwa miaka 15. Ametumika kwa uaminifu vijijini, mijini na katika majiji ya Tanzania kwa takriban miaka 40. Andrea, jina lake la kubatizwa, alistaafu kazi za mchungaji ili ahubiri Injili.

### Fahamu zaidi kuhusu AfriTWENDE!

Kwenye tovuti yetu, tuna matoleo matano ya Kiswahili! Kila toleo lina makala ambayo itakufundisha zaidi kuhusu umisheni, kukuarifu kuhusu kile wamisionari wanafanya shambani, na kukuchochea kuwa hodari katika imani yako. Unaweza kuona makala yote na kupakua masuala bila malipo kwenye tovuti yetu kwa www.afrigo.org/afritwende.

# AKINA MAMA WA MSAADA

## KUSIMAMA KWENYE PENGO KWA AJILI YA WATOTO WA WAMISHENARI

NA FURAHA KENGELA

Mnamo Februari 1996, bweni la watoto la EMS lilifunguliwa huko Jos, Nigeria, ili kuwapatia makazi watoto wa wamishenari wa EMS ambao walikuwa wakihudumu katika maeneo ya umisheni. Wazo hilo lilichochewa na kugundua kwamba asilimia 25 ya wamishenari waliacha umishenari kwa sababu ya ukosefu wa elimu bora kwa watoto wao. Kufikia mwaka uliofuata, bweni hilo lilikuwa limejaa, likiwa makazi kwa watoto 50. Matukio katika maadhimisho ya mwaka wa kwanza yalichochea kuzaliwa kwa shirika la kusaidia watoto la Akina Mama la EMS (EMS Children Support Mothers), ambalo baadaye likaitwa Support Mothers International (SMI).

Maadhimisho hayo yalifanyika katika viwanja vya shule ya wafanyakazi wa ECWA na kuleta pamoja watu wazima na watoto kutoka familia za SIM na EMS, waumini wa kanisa la ECWA, marafiki na watu wengine wenye kutakia wenzao mema. Kwa sababu bweni halikuwa na nafasi ya kuwahifadhi watoto wa wamishenari zaidi, tukio hilo lililenga kupata fedha kwa ajili ya upanuzi. Wake na watoto wa wamishenari wa SIM waliotoka ugenini walijitolea kuandaa viburudisho, na waliwahudumia wageni vizuri sana kiasi kwamba waliwagusa sana wanawake wa Nigeria waliohudhuria.

### Kuzaliwa

Dkt. Lami Bakari Ibrahim, mwanzilishi wa SMI, anakumbuka kwamba baada ya tukio hilo, baadhi ya wanawake wa Nigeria walibaki nyuma na kuulizana, "Kwa nini baada ya miaka 100 ya kuwa na wamishonari wa SIM katika nchi yetu, bado wanatutumikia? Vipi kuhusu sisi wanawake wa kitaifa? Tunaweza kufanya nini?" Uchunguzi wao ulisababisha mkutano wa ufuatiliaji ambapo walikaribisha changamoto ya kukusanya fedha ili kupanua uwezo wa bweni. Walizungumza na marafiki na watu wao wa karibu, na kukusanya pesa za kutosha kujenga jengo imara. Huu ulikuwa mwanzo wa Akina Mama wa Msaada kusimama katika pengo la wazazi kwa ajili ya watoto wa wamishenari. Walitoa chakula, nguo, vifaa vya kusafishia, na kadhalika. Baadhi ya Akina Mama waliwakaribisha nyumbani kwao watoto wakati wa (likizo) mapumziko ya shule na wengine walitembelea bwenini mara mbili kwa wiki kwa ajili ya kujumuika na kufanya shughuli pamoja nao. Kwa pamoja, walitengeneza vitu vya ufundi kama vile kuunda upya kadi za Krismasi za zamani na kupamba viatu au kanda mbili kwa shanga.


Picha ya wawakilishi

### Kukua

Akina Mama hawa walisafiri kote nchini ili kuleta ufahamu kwa watu kuhusu mahitaji ya watoto wa wamishenari wa EMS. Walichukua bidhaa za kutengeneza kwa mikono, ambazo sasa zina lebo, 'Mwana-Kondoo wa EMS,' na kuziuza ili kupata pesa wakati wowote walipopata nafasi ya kushirikisha mbele ya vikundi vya wanawake katika makanisa mengine. Baadhi ya watoto wa EMS walienda na kushiriki matukio hayo wakati Wamama hawa walipowashirikisha.

Dkt. Lami anaeleza kuwa akina mama hawapokei michango moja kwa moja. Wanashirikisha maono, na kutangaza mahitaji mbalimbali. Wanahimiza vikundi vya wanawake kutembelea bwenini na kujionea wenyewe maeneo yenye uhitaji wanayoweza kusaidia.

### Matunda

Dkt. Lami anaeleza kwamba ingawa kikundi hiki kwa sasa hakijachangamka kama hapo awali, malengo yote ya awali ya kukianzisha yalitimia. Sio tu kwamba walipanua bweni; pia walinunua ekari tisa za ardhi, wakaweka majengo ya shule na ya wafanyakazi, na kuanzisha shamba la mifugo. "Tuliona tulichofanya kama kuhudumu katika umisheni, ingawa hatukuwa shambani kama wazazi wao," Dkt. Lami anakumbuka. Kazi ya Akina Mama wa Msaada inaonyesha kwamba wakati wamishenari wanapohudumu kwenye mstari wa mbele, tukiwa kama familia ya kweli katika Kristo, sisi tulio nyumbani tunaweza kusimama katika pengo kwa njia za maana sana.



# MAKUNDI LA WATU: WABEJA WA ERITREA, SUDAN, NA MISRI

Kabila la Wabeja ni kundi la watu wanaohamahama ambao wamekuwa wakiishi katika nchi za Sudan, Eritrea, na Misri kwa zaidi ya miaka 4,000. Katika historia yao, waliukubali Uislamu na asilimia 99 ni Waislamu. Wanatekeleza Uislamu wa mchanganyiko na dini za asili na wanaamini katika jicho baya na majini. Wanajaribu kupata nguvu kutoka kwao kwa kutumia hirizi.

Wabeja ni kundi la watu ambao huonekana kama sio wa muhimu na ni maskini. Wakiwa ni idadi ya takribani watu milioni 4, wengi wao wana elimu ndogo au hawana kabisa na wanachukuliwa kuwa watu wa tabaka la chini na wananchi wenzao. Mazingira yao ya kuhamahama yanapungua na wengi wanahamia mijini kutafuta kazi za mikono na zenye malipo duni. Mtu asiyekuwa Mbeja atapendelewa kila wakati kuliko Mbeja wakati wa kuajiri.

Sababu moja ya kwa nini hawajafikiwa kabisa ni kwamba ili kuwafikia, mmishenari atalazimika kuishi katika mazingira magumu mbali na maeneo ya mijini. Huko nchini Sudan, Misri, na Eritrea, Wakristo wametambua kwamba Wabeja wanamhitaji Yesu, na wameanza kusikia msukumo wa kuwafikia. Kijana mmoja amehamia mahali pa mbali ili kuwafikishia injili. Wengine katika miji wameanza kutoa maji baridi au juisi kwa watu wa kundi la Wabeja ambao hupita karibu na kanisa lao. Wengine wameanza kupeleka chakula kwa wafungwa wa kabila au kundi la Wabeja.

Wabeja wanazidi kukatishwa tamaa na serikali za Kiislamu zinazojaribu kufuta utamaduni na lugha yao. Katika maeneo fulani, wanaomba shule za Kikristo kwa watoto wao na kuomba wamishenari. Walakini, idadi inayoufuata Ukristo bado ni ndogo sana.

## KWA KIFUPI

- Abu Nasr Mutahhar al-Maqdisi, aliandika katika karne ya kumi kwamba Wabeja walikuwa Wakristo wakati huo.
- Wabeja hufunga ndoa kati ya mtu na binamu yake.
- Baadhi ya Sehemu tu za Maandiko ziko katika lugha yao ya Bedawiyet.

## OMBA KWA AJILI YA

- Maandiko zaidi na nyenzo zitafsiriwe kwenda lugha yao ya Bedawiyet.
- Wakristo wenyeji wasikie msukumo wa Roho Mtakatifu na kuwafikia Wabeja.
- Wabeja wamjue Yesu na kuanza harakati miongoni mwa watu wao.

Vyanzo: http://bejafriends.org/ • https://joshuaproject.net/people_groups/10766 • https://omniglot.com/writing/beja.htm
https://en.wikipedia.org/wiki/Beja_people

SIM By Prayer
AFRICA INLAND MISSION

**AFRITWENDE**: afritwende@afrigo.org **AFRIGO**: info@afrigo.org **ALLONS-Y !** : info@afrigo.org **AFRÍDE**: afride@afrigo.org

**SIM Afrika Mashariki**
**Sm:** +251 911 206 530
east-africa.office@sim.org

**SIM Afrika Magharibi**
Sm: +233 30 222 5225
wamo.personnel@sim.org

**SIM Kusini mwa Afrika**
Tel: +27 21 7153200
za.enquiries@sim.org

**AIM Kimataifa**
amc.io@aimint.org
aimint.org/africanmobilization/